KISWAHILI

MTIHANI WA KARATASI YA 1

Soma ufahamu unaofuata halafu ujibu maswali.

Watu wengi hushangaa jinsi ulimwengu unavyobadilika kwa mwendo wa kasi. Maendeleo yanazidi kushuhudiwa katika sekta za kiuchumi, kisiasa na kijamii. Hata hivyo, ni dhahiri kuwa maendeleo haya yameiletea jamii manufaa na madhara.

Sekta ya kijamii imekumbwa na mabadiliko si haba. Hapo awali, jamii nyingi ziliienzi na kuikumbatia mienendo ifaayo. Mtoto aliyeonyesha dalili za kupotoka, kwa mfano, alikashifiwa vikali sio tu na wazazi au walezi wake bali na jamii nzima. Mtoto alikuwa mali ya jamii. Kwa sababu hiyo, jamii ilimwelekeza ilivyostahili ikifahamu kuwa, mtoto umleavyo ndivyo akuavyo. Katu jamii haikumdekeza mtoto, bali ilimrudi aliyekosa papo hapo.

Inasikitisha kuona jinsi ambavyo mambo yamebadilika kwa upande wa mavazi. Yami kuwa mazoea kwa baadhi ya waja kuvalia mavazi yanayowaacha nusu uchi! Isitoshe, wengine wao hujipiga picha na kuzisambaza kwenye mitandao bila soni. La ajabu ni kwamba, wanaofanga hivyo ni wakubwa kwa wadogo, wake kwa waume.

Kwa upande mwingine, baadhi ya vijana huwavunjia heshima wakubwa wao. Utawapata katika matwana wameziba masikio yao kwa vidude hata wanapoombwa kiti na mzee hawasikii. Nayo lugha wanayoitumia kuwasiliana na wazee hawa imekosa adabu. Sikwambii vituko wanavyovifanya hadharani. Ajabu! Wanaenda kinuume cha mila na desturi za jamii zao na kusahau kuwa mwacha mila ni mtumwa.

Ukweli ni kwamba, uadilifu ni muhimu kwa mtu yeyote. Maadili hayafai kupuuzwa eti kwa sababu ya maendeleo. Watu wote wanafaa kuwa na mienendo inayokubalika katika jamii. Maendeleo yawe njia ya kuendeleza jamii bali si ya kuididimiza.

1. Kulingana na aya ya kwanza, ni kweli kuwa watu;
    A. wote hushangaa jinsi ulimwengu unavyobadilika kwa kasi.
    B. wengi hushangaa jinsi ulimwengu unavyobadilika.
    C. wengi hushangaa jinsi ulimwengu usivyobadilika kwa kasi.
    D. wengi hushangaa jinsi ulimwengu unavyobadilika kwa haraka.
2. Kauli kuwa 'maendeleo haya yameiletea jamii manufaa na madhara' inaweza ikarejelewa kwa methali gani?
    A. Hakuna masika yasiyokuwa na mbu.
    B. Hakuna marefu yasiyokuwa na ncha.
    C. Hakuna msiba usiokuwa na mwenziwe.
    D. Hakuna kubwa lisiloshindwa.
3. Mwandishi anasema kuwa maendeleo yanazidi kushuhudiwa katika sekta zifuatazo isipokuwa;
    A. sekta ya kiuchumi
    B. sekta ya kisiasa
    C. sekta ya kijamii
    D. sekta ya kilimo
4. Kulingana na aya ya pili, ni kweli kwamba;
    A. mabadiliko haba yametokea katika sekta ya kijamii.
    B. kila mtoto alikashifiwa vikali.
    C. jamii nzima ilichangia katika malezi ya mtoto.
    D. mtoto hakuwa na nyumbani kwao.
5. Kwa nini mwandishi anasema kuwa mabadiliko yametokea katika upande wa mavazi?
    A. Kwa kuwa inasikitisha kuona mabadiliko hayo
    B. Kwa kuwa watu wengine huvalia mavazi yanayowaacha nusu uchi